**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019

*[Imeandikwa kwa mujibu wa Kanuni ya 123 na kuwasilishwa Bungeni kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

IDARA YA KAMATI ZA BUNGE,
S.L.P. 941,
**DODOMA**.

**23 APRILI, 2018**

**YALIYOMO**

**SEHEMU YA KWANZA** .......... **1**

**1.0 UTANGULIZI** .......... **1**

**SEHEMU YA PILI** .......... **3**

**2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019** .......... **3**

2.1 Makusanyo ya Mapato .......... 3

2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2017/2018 .......... 3

2.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2017/2018 .......... 4

2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati .......... 6

**2.5 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019** .......... **9**

2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 .......... 9

2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 .......... 10

2.5.3 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2018/2019 .......... 11

**SEHEMU YA TATU** .......... **19**

**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI** .......... **19**

3.1 Sekta ya Uchukuzi .......... 19

3.2 Sekta ya Ujenzi .......... 24

3.3 Sekta ya Mawasiliano .......... 29

**4.0 HITIMISHO** .......... **31**

4.1 Shukrani .......... 31

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo:-

   i. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

   ii. Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu manne ambayo ni Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa

Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Mambo mengine yaliyojitokeza wakati wa kujadili, kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

c) Sehemu ya Tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi), Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi) na Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano).

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 2.1 Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, fungu 68- Sekta ya Mawasiliano ilikusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 2,200,000.00**; na **shilingi 10, 907,180,261.25** kutoka huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Februari, 2018. Aidha, makusanyo mengine ya Sekta ya Mawasiliano ni kutokana na mfumo wa *TTMS* ambapo ilikusanywa kiasi cha **shilingi 8,716,083,646.58.**

**Mheshimiwa Spika**, fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 62,002,000.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Hadi kufika mwezi Machi, 2018 jumla ya **Shilingi 26,120,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 42.13** ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa.

### 2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia Machi, 2018**

| SEKTA | Fedha zilizoidhinishwa 2017/18 | | | Fedha zilizotolewa hadi Machi, 2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mishahara na Matumizi Mengineyo | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo | Mishahara na Matumizi Mengineyo | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo |
| Uchukuzi | 91,142,025,000 | 2,227,646,000,000 | 250,285,182,000 | 53,591,490,874.54(58%) | 974,444,280,000 (44%) | 4,365,400,000(1.74%) |
| Ujenzi | 36,032,513,782 | 1,865,443,630,496.20 | 545,582,432,000 | 22,904,459,689.2(0 (63.57%) | 1,375,064,099,005.54 (74% ) | 237,882,582,514 (44%) |
| Mawasiliano | 4,104,139,000 | 14,000,000,000 | 0 | 2,340,691,977 (57.03%) | 0 | 0 |

*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2017/2018*

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa sekta ya Ujenzi ni wakuridhisha kwani hadi mwezi Machi, 2018 **asilimia 74** ya fedha za ndani za Miradi ya Maendeleo ilikuwa imeshatolewa.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni tofauti na ilivyo katika Sekta ya Uchukuzi ambako utolewaji wa fedha siyo wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 fedha zilizotolewa hazizidi **asilimia 45**. Hali ni mbaya zaidi kwa Sekta ya Mawasiliano ambayo katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilitengewa **shilingi bilioni 14** na hadi mwezi Machi, 2018 **hakuna** fedha zilizotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokutolewa kwa wakati kwa fedha za miradi ya maendeleo katika sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano imekuwa ni changamoto kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 baadhi ya miradi haikuwa imepata fedha yoyote. Miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya Mtwara-M/bay, Mchuchuma & Liganga (Km 1092), ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tanga-Arusha hadi Musoma (Km 1,108), kuboresha miundombinu ya Chuo cha Taifa cha usafirishaji-NIT na mradi wa usafiri wa treni Dar es Salaam. Miradi mingine ni pamoja na mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Kituo cha Kutengeneza Vifaa vya TEHAMa na Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

## 2.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 21 Machi, 2018 ambapo Kamati iliweza kutembelea baadhi ya miradi ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi katika Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Simiyu.

**Mheshimiwa Spika,** jedwali lifuatalo linaonesha miradi iliyokaguliwa ikihusisha fedha zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 na fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Kamati ilipotembelea miradi hiyo.

**Jedwali Na. 2, Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa na Kamati, Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2018**

| Na | Fungu | Jina la Mradi | Fedha za Miradi zilizoidhinishwa 2017/18 | | Fedha za Miradi zilizotolewa hadi Machi, 2018 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Ndani** | **Nje** | **Ndani** | **Nje** |
| 1 | 98-Ujenzi | 4130- Barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora | 75,381,000,000 | 15,081,000,000 | 79,226,930,000 | - |
| | | 4112- Ujenzi wa barabara ya Kigoma-Kidawa-Uvinza-Kaliua | 72,782,000,000 | - | 43,850,000,000 | - |
| | | 4152-Barabara ya Tabora -Nzega | 90,801,263,263 | - | 46,011,000,000 | - |
| | | 4162- Ujenzi wa barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi-Lamadi | 192,389,350 | - | 58,642,889,350 | - |
| | | 4155- barabara ya Nyanguge – Musoma-Kisesa bypass | 948,407,289 | - | 40,594,497,841 | - |
| | | 4209- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza | 9,300,820,927 | - | 15,000,000 | - |
| | | 4295 barabara ya Dodoma - Manyoni | 145,466,784,269 | - | 145,451,780,000 | - |
| 2 | 62-Uchukuzi | 4230-Mradi wa ukarabati wa Bandari ya Mwanza | 6,295,000,000 | - | - | - |
| | | 4295- Ukarabati wa Meli katika Ziwa Victoria | 24,496,000,000 | - | 24,496,000,000 | - |

*Chanzo; Taarifa ya Kamati ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2017/2018*

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyobainika katika ziara hiyo:-

a) Mradi wa ujenzi na upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Mwanza, hadi Kamati ilipotembelea mradi huu, kati ya **shilingi bilioni 9, 300, 820, 927** fedha za ndani kwa ajili ya kumalizia kazi ya ujenzi wa jengo jipya la kuongezea ndege, kurefusha barabara ya kutua na kuruka ndege, upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa uzio, ujenzi wa jengo la mizigo, usimikaji wa taa za kuongozea ndege, kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na miundombinu yake pamoja na barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho yake. Hadi

Kamati ilipotembelea mradi huu, **shilingi milioni 15,000,000** tu zilikuwa zimetolewa.

b) Mradi wa uboreshaji wa bandari ya Mwanza, uliidhinishiwa **shilingi bilioni 6, 295,000,000** mwaka wa Fedha 2017/18 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari katika Ziwa Victoria. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu hakuna fedha yoyote iliyotolewa.

c) Mradi wa Ukarabati wa Meli katika ziwa Victoria ambao una lengo la kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu yaani (Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa) kwa kununua meli mpya na kukarabati zilizopo. Kamati inaipongeza Serikali kwani imetoa kiasi chote cha fedha kilichokuwa kimeidhinishwa cha **shilingi bilioni 24,496,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa miradi hasa ya sekta ya Uchukuzi ni kutokupatikana fedha za miradi kwa wakati.

## 2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, Barabara na Mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na:-

a) Ushauri wa kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam ili iweze kuvutia wateja wengi na kushindana na bandari zingine.

   i) Kamati imejulishwa kuwa baadhi ya tozo zilizokuwa kikwazo kwa wafanyabiashara zimeangaliwa na kufutwa. Mfano, Serikali imefuta tozo ya ongezeko la thamani kwa huduma zitolewazo na mawakala kwa wenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani *(VAT on transit goods);*

ii) Himaya ya Forodha kwa Pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mzigo wa Congo, Mpango huu umesitishwa kuanzia tangu tarehe 28 Februari 2018;

iii) Wadau wote wa bandari sasa hufanya kazi saa 24 kwa siku zote za juma, hii imesaidia kupunguza muda wa mzigo kukaa bandarini;

iv) Mradi wa upanuzi na uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam; shughuli mbalimbali zimeendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na tafiti na usanifu wa mradi Gati Na. 1-7 ambapo tafiti na usanifu kwa Gati Na. 1-3 umekamilika;

Aidha, ujenzi wa gati la kuhudumia meli za magari (RoRo berth) umeanza kwa kujaza kifusi na kuondoa maji;

Vilevile kuhusu upanuzi wa lango la kuingia bandarini, tathmini ya zabuni ya awali imekamilika na ripoti imewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya idhini. Aidha, tathmini ya zabuni ya kumpata Mtaalam Mwelekezi imekamilika;

Kuhusu ujenzi wa Gati Na. 13&14, Kamati imejulishwa kuwa mradi huu utatekelezwa katika awamu ya pili ya mradi wa kuboresha bandari ya Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya kuondolewa kwa baadhi ya tozo kumeongeza shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi jirani za Burundi, Jumhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia ambapo katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda kwenye nchi hizo ilikuwa ni tani milioni 3.864 zikilinganishwa na tani milioni 3.143 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017.

b) Ushauri wa kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake yote;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefamishwa kuwa ujenzi wa reli hii ya kati kwa kiwango cha Kimataifa unaendelea kwa awamu. Awamu ya kwanza

utekelezaji wake umefikia asilimia tisa (9%) kutoka Dar es Salaam-Morogoro (km 205) na unatarajia kukamilika Novemba, 2019;

Aidha, Awamu ya pili ya kutoka Morogoro-Makutopora (km 336), Mkataba umesainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na jiwe la Msingi kuwekwa tarehe 14 Machi, 2018 ambapo unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2020;

c) Kuunganisha RAHCO na TRL, ushauri umezingatiwa ambapo mnamo tarehe 28 Februari 2018 Shirika la Reli Tanzania-TRC lilianzishwa rasmi ikiwa ni matokeo ya kuunganishwa kwa Makampuni hayo mawili;

d) Serikali kulipa madeni ya wafanyakazi wa TAZARA; Kamati imejulishwa kuwa kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha Julai, 2017 hadi Desemba, 2017 jumla ya **milioni shilingi 550, 708,500** zimelipwa;

Aidha, kuhusu ushauri wa kurekebisha gharama za usafirishaji ili kwavutia wafanyabiashara wengi kutumia TAZARA; Suala hili limezingatiwa ambapo bei ya kusafirisha Shaba inayotoka DRC kuja Dar es Salaam imepungua kutoka **Dola za Marekani 110** hadi **90** kwa tani. Aidha, kusafirisha shaba kutoka Ndola Zambia kuja Bandari ya Dar es Salaam bei imepungua kutoka **Dola za Marekani 90** hadi **80** kwa tani. Punguzo hili limefanyika hata kwa mizigo ya ndani kama vile mbao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia ushauri huo wa Kamati, TAZARA imeweza kuwa na ufanisi ambapo katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Februari 2018 ilisafirisha shehena ya **tani 146, 474** ambapo lengo lilikuwa ni kusafirisha **tani 200,000** kwa mwaka 2017/18. Utendaji huu ni sawa na **asilimia 73.2** ya lengo lililokuwa limewekwa ukilinganishwa na kipindi cha mwaka 2016/17 kilichoanzia Julai 2016 hadi Januari ,2017 ambapo shehena ya **tani 93,688** zilisafirishwa.

e) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha viwanja vyote vinapatiwa hati miliki, hati miliki zimeendelea kutolewa kwa viwanja vya vya KIA, Kigoma, Bukoba na Songwe;

f) Kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami; baadhi ya barabara hizo zimeanza kufanyiwa kazi Mfano, barabara ya Mpanda-Uvinza-Kasulu-Kibondo hadi Nyakanazi inayounganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma na Katavi, ujenzi wa barabara ya Njombe- Ndulamo-Makete (km 107.4)ambapo inaunganisha Mkoa ya Njombe na Mbeya, barabara ya Mbinga- Mbamba Bay (km 67) na Mpemba-Isongole (km 51.2);

g) Kupunguza athari za matuta ya barabarani, baadhi ya matuta yameendelea kuondolewa na kupunguzwa ili yawe katika vipimo sahihi kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa usanifu wa barabara wa mwaka 2011 (*Road Geometric Design Manual*) ya Mwaka 2011;

h) Kuongeza mizani za kisasa zinazopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo; Kamati imejulishwa mizani hizo za kisasa zinaendelea kujengwa katika maeneo mengine kama vile Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe);

i) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA kuharakisha kupata ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu kwa kutumia mtambo wa *Telecommunication Traffic Monitoring System-TTMS* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu za mkononi; Kamati imejulishwa kuwa uboreshaji Mfumo wa *TTMS* wa "*Module"* ya kuhakiki mapato ya huduma za mawasiliano umefanyika na tayari takwimu za huduma za mawasiliano zinatolewa na Kampuni za Vodacom, Tigo na Airtel.

## 2.5 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hususan Sekta ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya

**shilingi milioni 45,002,000.00** kutoka Idara zenye vyanzo vya mapato kama vile Idara ya Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi, Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi.

### 2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 4.2 (4,270,879,381,344)**. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa:-

**Jedwali Na.3, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

| SEKTA | MATUMIZI YA KAWAIDA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|
| **Ujenzi** | 42,898,011,066 | 1,822,093,269,000 | **1,864,991,280,066** |
| **Uchukuzi** | 86,292,678,278 | 2,300,739,000,000 | **2,387,031,678,278** |
| **Mawasiliano** | 3,856,423,000 | 15,000,000,000 | **18, 856, 423, 000** |
| **JUMLA KUU** | **133,047,112,344** | **4,137,832,269,000** | **4,270,879,381,344** |

*Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019*

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2018/2019 ambayo ni **trilioni 4.2** imeshuka kwa **asilimia 7** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha uliopita wa 2017/2018 ambayo ilikuwa **trilioni 4.5.**

### 2.5.3 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2018/2019

a) **Sekta ya Uchukuzi**

i. **Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** katika mipango ya Sekta ya Uchukuzi ya Mwaka 2018/2019, miongoni mwa malengo yaliyowekwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu ya reli nchini hususan reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge).*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ujenzi wa reli ya kati kutoka **shilingi bilioni 900** zilizoidhinishwa 2017/2018 hadi **shilingi trilioni 1.4** zilizotengwa kwa mwaka 2018/19. Ongezeko hili la **asilimia 64** ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) na Morogoro hadi Makutopora (km 336).

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba wa awamu ya pili ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Morogoro hadi Makutopora ambapo mkataba ulisainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na Kampuni ya **Yapi Merkezi ya Uturuki**. Aidha, jiwe la msingi liliwekwa tarehe 14 Machi 2018 ambapo gharama za mradi ni **shilingi trilioni 4.3.**

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na mali ghafi hatimaye kuchochea ukuaji wa viwanda, na hata kuongeza Pato la Taifa.

Ni matarajio ya Kamati kuwa reli hii itajengwa na matawi yake kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika maeneo ambayo yana mali ghafi nyingi ili reli hii iweze kufanya kazi ipasavyo na kuwa na tija.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati imejulishwa kuwa zimetengwa **shilingi bilioni 6.5 (6, 500,000,000.00)** kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli ya kisasa kati ya Mtwara- Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Tanga-Arusha-Musoma, pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ikijumuisha njia mpya ya reli katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, zimetengwa **shilingi bilion 252,639,000,000** kwa ajili ya Mfuko wa reli.

ii. **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Bandari Tanzania ina majukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia Sekta binafsi katika kuendeleza bandari. Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za Maziwa makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi; pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa nia na dhamira ya Serikali ya awamu ya tano ni kuwa na uchumi wa Viwanda; ni rai ya Kamati kuwa wakati Mamlaka ya Bandari inaendelea kuboresha, kukarabati na kujenga Bandari ya Dar es Salaam; pia ianze ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na bandari ya Ziwa Nyasa.

iii. **Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha dhamira ya dhati ya kufufua Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ambapo mnamo Mwezi Machi, 2018 imepokelewa ndege mpya ya tatu aina ya Bombadia D8- Q400. Ujio wa ndege hii umeifanya nchi yetu kuwa na ndege nne. Katika kuendeleza juhudi hizo

mwaka wa fedha 2018/2019 imetengwa **shilingi bilioni 495,600,000,000** kwa ajili ya kuboresha Kampuni ya Ndege ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, wakati tunaendelea kuongeza idadi ya ndege zilizosalia, ni vyema kuendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazolikabili shirika letu kama vile;-

a) Uhaba wa rasilimali fedha;
b) Upungufu wa wataalam hasa marubani na wahandisi ambao wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu;
c) Kuchelewa kurejea katika Chama cha Mashirika ya Ndege Duniani (IATA); na
d) Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Katavi kutokana na mapungufu katika viwanja hivyo ikiwemo ukosefu wa magari ya zima moto na namba ya usajili wa Kiwanja.

b) **Sekta ya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo

ni kuwezesha barabara zetu ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

i. **Miradi ya ujenzi wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri zinazoendelea kutekelezwa za ujenzi wa barabara nchini, changamoto kubwa imekuwa ni rasilimali fedha ambapo kuchelewa kwake mara nyingine kumesababisha gharama za miradi kuongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara

za lami ifikapo mwishoni mwa 2017/18 bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya –Makete- Njombe, Lindi- Morogoro,Lindi-Ruvuma n.k. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

ii. **Mizani za Barabarani**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara (TANROADS) ndio imepewa jukumu la kusimamia utendaji kazi za udhibiti wa uzito wa magari barabarani ambapo hadi sasa Wakala huu unamiliki jumla ya mizani 60 ambapo 38 ni ya kudumu, 22 inahamishika na mizani 3 zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo. Pamoja na kuwa na vituo vingi vya kudhibiti uzito wa magari, bado changamoto ya uharibifu wa barabara kutokana na uzito uliopitiliza wa magari imeendelea kuwepo na kuligharimu Taifa fedha za kufanya ukarabati wa barabara hizi mara kwa mara. Kamati inaona kuna umuhimu sasa wa kutafuta suluhu ya changamoto hii ili kunusuru barabara zetu na hatimae ziweze kudumu kwa muda mrefu.

iii. **Fedha za Mfuko wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mijini na vijijini kwa uwiano wa asilimia 20 kwa barabara za vijijini na asilimia 80 kwa barabara kuu.

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa malengo hayo hayo mazuri ambapo Mwaka, 2017, Serikali ilianzisha Wakala wa Barabara Vijijini -TARURA chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI kwa ajili ya kuhudumia barabara zote zilizoko vijijini kwa mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara ambapo sasa TARURA inapata mgao wa asilimia 30 na TANROADS inapata mgao wa asilimia 70.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ya Viwanda haitowezekana ikiwa barabara hizi za vijijini ambazo nyingi zipo katika hali mbaya na hazipitiki hazitoangaliwa kwa jicho la pekee na kwa haraka ili kurahisisha usafirishaji wa mali ghafi na binadamu. Hii ndio sababu Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia na kuangalia upya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa barabara.

iv. **Malipo ya Madai ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wakandarasi na Wahandisi Washauri katika ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2018 deni la Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara ni **shilingi bilioni 711.13**. Madeni yaliyolipwa ni yale yaliyohakikiwa hadi mwezi Juni, 2017. Aidha kazi ya kuhakiki madeni ya hadi mwezi Juni, 2017 imekamilika na fedha zinaendelea kutolewa kwa ajili ya malipo ya madai ya miradi ya barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha wakandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara. Kamati ilipokuwa katika ziara yake ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo mwezi Machi, 2018 ikiwa Mkoani Tabora, ilifarijika kukuta Wakandarasi watatu walioungana ambao wamepewa kazi ya ujenzi wa barabara kwa kipande cha barabara ya lami yenye kilometa 28 kutoka Urambo kwenda Kaliua. Hili ni jambo la kujivunia kwani imezoeleka kuwa miradi hii mikubwa yenye kuhitaji fedha nyingi inafanywa na wageni kutoka nje huku wazawa wakisaidia kazi ndogo ndogo tu.

Ni imani ya Kamati kuwa wakandarasi hao watafanya kazi yenye ubora na hatimae kuongeza imani kwa Serikali ili waweze kupewa kazi zingine.

v. **Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Machanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengenezo ya magari, mitambo, pikipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu unachangamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa rasilimali watu wenye ueledi wa kwenda samabamba na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kisasa vinavyoweza kuendana na magari, mitambo ya kisasa

ambayo inahitaji kutumia mashine ili kugungua tatizo wakati wa ukarabati na sio kufanya kazi kwa kubahatisha ambako kunatumia muda mwingi na gharama kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo magari ya Serikali yanakwenda kutengenezwa kwa waagizaji wakubwa *(dealer)* ambao gharama zao zinatozwa kulingana na muda ambao umetumika kutengeneza gari husika na hivyo kusababisha gharama kuwa kubwa.

vi. **Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa viwanja vya ndege ni muhimu sana hasa ukuzingatia wakati huu ambapo tunajivunia kuwa na ndege zetu wenyewe. Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano; katika mwaka wa fedha 2017/18 viwanja vya ndege vifuatavyo viliidhinishiwa fedha ambapo hadi kufika mwezi Machi, 2018 baadhi vilikuwa vimepata fedha kidogo na vingine vilikuwa hajijapata fedha kabisa. (Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kiliidhinishiwa **shilingi mioni 7,250** zimetolewa **shilingi 215,105,663)**, (Songwe- kati ya **shilingi milioni 230** zimetolewa **shilingi milioni 10** tu), (Mtwara- kati ya **shilingi milioni 1,150** zimetolewa **shilingi milioni 576**), (Sumbawanga -kati ya **shilingi milioni 13, 700** hakuna fedha zilizotolewa, (Kilimanjaro kati ya **shilingi milioni 27,868** hakuna fedha zilizotolewa) (Mpanda- kati ya **shilingi milioni 300)** na (Mwanza- kati ya **milioni 9,300** zimetolewa **milioni 15** tu).

**Mhshimiwa Spika**, kutokutolewa fedha za miradi hii kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na mabadiliko viwango vya kubadilisha fedha.

c) **Sekta ya Mawasiliano**

i. **Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta**

**Mheshimiwa Spika**, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu umeendelea kuwa changamoto. Mfano, katika Mwaka wa Fedha uliopita 2016/2017 Mradi huu uliidhinishiwa **shilingi bilioni 3** ambapo kiasi kilichotolewa kilikuwa **milioni 95, 154, 500** sawa na **asilimia 3**. Na katika mwaka wa fedha wa 2017/18 mradi huu uliidhinishiwa **shilingi billion 3** ambapo hadi kufikia Machi 2018, hakuna kiasi chochote kilichotolewa.

Ni matarajio ya Kamati kwamba mradi huu sasa utapewa kipaumbele na fedha zilizoidhinishwa zitatolewa ili kkuharakisha maendeleo katika taifa letu.

ii. **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF)**

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba, 2017, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kuona hali ya huduma za mawasiliano zinavyopatikana kwa sehemu ambazo minara ilijengwa na makampuni ya simu kwa kutumia ruzuku kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-*UCSAF*. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea takribani Mikoa 20 ya Tanzania Bara, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo;-

a) Serikali za Mikoa, Wilaya pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya simu yenyewe; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa;

b) Upungufu wa rasilimali watu kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuweza kufuatilia kwa karibu ujenzi wa minara unaofanywa na Makampuni ya Simu;

c) Makampuni ya simu kutokutoa huduma za kijamii katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibiashara;

d) Migogoro dhidi ya umiliki wa maeneo husika;

e) Wizi wa vifaa vya minara kama vile mafuta, betri na nyaya aina ya ''*fiber*";

f) Minara mingi iliyojengwa inatumia umeme wa jua (*solar power*), hii inasababisha nyakati za usiku hasa kipindi cha mvua maeneo mengi kuwa na mawasiliano hafifu kwa sababu jua haliwaki kipidi kirefu;na

g) Makampuni kujenga minara pasipo kuweka huduma za kijamii kama vyoo, kibanda cha mlinzi na huduma zingine za msingi kwenye maeneo la mnara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa rai ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Pamoja na juhudi za Serikali kutoa ruzuku kwa kampuni za simu ili ziweze kufikia maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara, Kamati imebaini kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajahimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo hayo.

iii. **Kampuni ya Simu Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha kituo cha kisasa cha Kanzi Data ya Taifa kwa njia ya mtandao (*Internet Data Center*) ambacho kilianza kufanya kazi tangu mwezi Agosti, 2016. Hiki ni kituo chenye uwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu kwa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, Mashirika Binafsi na hata Watu Binafsi. Kamati imebaini kutokuwepo kwa hamasa kwa Serikali na Taasisi/Mashirika yake kwani mpaka sasa ni taasisi 41 tu ndizo zinazotumia kituo hiki.

Hofu ya Kamati ni Taasisi na Mashirika ya Umma kuendelea kujenga vituo vingine kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake wakati kituo hiki kipo na kinauwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu hizo. Taasisi kama vile Bunge inaweza kutunza taarifa rasmi za Bunge *(Hansard),* vilevile Mahakama inaweza kutumia kituo hiki kwa kutunza na mashauri yaliyokwisha tolewa uamuzi kwa mahakama *(Judgement*).

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Ushauri huu wa Kamati umezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo nchini. Ni matarajio ya Kamati kuwa, fedha zilizotengwa kwa Sekta zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka 2018/2019, zitatolewa kwa wakati ili kuharakisha maendeleo.

### 3.1 Sekta ya Uchukuzi

1) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu ujenzi wa reli nchini;

a) Kamati bado inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora – kigoma - Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema; na Tabora- Mwanza;

Ikumbukwe kuwa, licha ya kuwa reli hii itakuwa ikihudumia na kunufaisha takribani Mikoa 15 ya Tanzania Bara kwa kusafirisha mizigo na abiria, pia itasaidia sana kusafirisha mizigo mingi kwenda nchi jirani kama vile DR Congo, Burundi na Rwanda.

Aidha, ujenzi wa reli hii uende sambamba na kudhibiti maeneo korofi kama vile Gulwe na Godegode- Kilosa. Vilevile kuimarisha karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu;

b) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vema sasa Shirika la Reli Tanzania-TRC kuweka alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;

c) Shirika la reli kuanza kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;

d) Kwa kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ni wa gharama kubwa, na kwa kuwa pamoja na ujenzi wa reli ya kati unaoendelea sasa, pia tunatarajia kuanza kujenga reli zingine za Tanga –Arusha –Musoma (1108 km), Mtwara- Mbambabei na Mchuchuma Liganga (1092 km) na Isaka –Rusumo (371). Kamati inashauri Serikali kujenga reli hizi kwa awamu kwa kufuata kipaumbele; na

e) Ili kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini, Serikali iangalie uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi au kupata mikopo yenye gharama nafuu. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kuendelea kutoa huduma zingine muhimu kwa kutumia fedha zake za ndani.

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari;

a) Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kubakisha angalau **asilimia 40** ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake;

b) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza upanuzi na ukarabati wa bandari ya Dara es Salaam pamoja na kukamilisha kituo cha pamoja cha huduma kwa wateja (*one stop centre)*, hata hivyo, ili kuongeza ufanisi na mapato katika bandari ya Dar es Salaam, Kamati bado inasisitiza kufanyika juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha gati la mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga gati namba 13 na 14;

c) Wadau wote wa bandari kuunganishwa kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau

wengine kama Mkemia mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-TBS ,Wizara ya Nishati na Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo;

d) Mchakato wa kuwa na eneo Kurasini-Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika;

e) Serikali kuendelea kuondoa vikwazo visivyo vya lazima katika Bandari nchini ili kuzidi kuvutia na kujenga mazingira ya wafanyabiashara wengi kutumia Bandari zetu;

f) Serikali kuharakisha ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda mrefu sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Katosho-Kigoma na Misungwi –Mwanza;

g) Kamati inashauri Serikali kuharakisha majadiliano na wabia ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwani kukamilika kwa bandari hii kutatoa fursa nyingi za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali kulipa fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kampuni ya Huduma za Meli kupanga mipango ya kujiendesha kisasa kwa kuimarisha njia za ukusanyaji mapato kwa njia kielektroniki, kuweka teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli (*Flow Scanner)* na kuweka mfumo wa kuweza kufatilia mahali meli ilipo kila wakati (*trucking system)*. Kufanya haya kutasaidia kuweza kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni;

b) Kampuni ya Meli Tanzania kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na Reli kwani kufanya hivyo kutawezesha kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara kuweza kusafirisha mizigo toka Dar es salaam mpaka

Uganda na hatimaye kupunguza gharama kwa wafanyabiashara na kuongeza pato na hata Kampuni hii kuweza kutoa gawio la faida kwa Serikali;

c) Serikali kujipanga kutengeneza Meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara na hata kuweza kulipa madeni yote inayodaiwa;

d) Serikali ihakikishe inalipa deni la mishahara ya miezi 23 kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kujiendesha kwani uwekezaji unaofanyika kwa sasa wa kukarabati na kujenga meli mpya katika Maziwa Makuu hautakuwa na tija ikiwa maslahi ya wafanyakazi hususani mishahara haitopewa kipaumbele; na

e) Serikali kurasimisha bandari bubu zilizozagaa katika mwambao wa Ziwa Victoria ili kuongeza mapato katika halmashauri na bandari kwa ujumla.

4) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Nchi wabia wa reli ya TAZARA kuendelea na mazungumzo ya kuimarisha reli hii kwani bado mahitaji yake ni makubwa kwa uchumi. Kamati inaamini kwa takwimu zilizopo za shehena inayotoka Bandarini peke yake na kusafirishwa na reli ya TAZARA inatosha kabisa Mamlaka hii kuweza kupata uwezo wa kujiendesha kibiashara kwani zipo zaidi ya tani 1,500,000 ambazo zinahitaji kusafirishwa kupitia reli hii;
b) Serikali kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha ili kuweza kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;

c) Serikali ijenge kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha; na

d) Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kendelea kulipa deni lote linalodaiwa na TAZARA.

5) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA:-

a) Ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- TAA iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi katika viwanja vya ndege nchini; Kamati inashauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli (*retention)* yatokanayo na viwanja vya ndege;

b) Kwa kuwa yapo mashirika mengi kama Ethad, Fly Dubai, Rwanda Air,Jambo Jet ya Kenya yanayofanya safari za kimataifa na yameonyesha nia ya kufanya safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; Kamati inashauri kuwahi kukamilishwa kwa jengo la kuongozea ndege *(tower),* jengo la mizigo, pamoja na kuondoa mapungufu mengine yanayokikabili kiwanja hiki ili kiweze kutumiwa na ndege za kimataifa na kuweza kuongeza mapato; na

c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kulipa fidia ili kumaliza migogoro na wanachi walio kwenye maeneo ya viwanja vya ndege. Vile vile kuharakisha zoezi la kupata Hati Miliki kwa viwanja vyote vya ndege na kuondokana kabisa migogoro hiyo katika siku za mbele.

6) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL,

a) Kampuni ya ndege ya Tanzania kuingia kwenye mfumo wa (*International Air Transport Assoacition) IATA* ili kuweza kufanya "*booking"* za abiria wanaotoka nje ya nchi wanapotaka kuunganisha ndege ndani ya Tanzania, jambo ambalo kwa sasa halifanyiki;

b) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja mara kwa mara ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote; Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga; na

c) ATCL ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi.

7) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini-SUMATRA:-

a) Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa nchi kavu na majini kuimarisha usalama na ubora katika kutoa huduma za usafiri kwani wimbi kubwa la ajali zinazotokea ni dalili tosha kuwa kuna mapungufu kwenye usimamizi wa sheria za usalama barabarani;na

b) Serikali kupitia SUMATRA kuhakikisha inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi kama vile Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Miji hii imekuwa ikikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha kutumia muda mwingi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

## 3.2 Sekta ya Ujenzi

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Barabara- TANROADS, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Serikali kutekeleza Sera yake ya kuunganisha Mikoa kwa barabara za lami (*Trunk Roads)* kama vile Lindi –Morogoro, Morogoro-Mlimba-Madeke Njombe, Lindi –Songea, Kigoma –Katavi-Tabora-Kigoma, Mbeya-Makete-Njombe, Arusha –Mara Aidha, miradi ya barabara hizi ambayo inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu. Vilevile, Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine *(Boarder Roads)* hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;

b) Serikali iangalie upya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara na kuongeza asilimia ya fedha zitolewazo kwa TARURA kufikia **asilimia 40** na Wakala wa Barabara Tanzania- TANROADS kupewa **asilimia 60**. Hii ni kutokana na ukweli kuwa barabara nyingi za vijijini hazipitiki katika misimu yote, na kwa kuwa Serikali inatekeleza Sera yake ya Viwanda ni vema kuongeza fedha kwa ajili ya barabara za vijijini ili ziweze kujengwa na kusafirisha mali ghafi zinazotoka vijijini kuja kwenye viwanda ambavyo vilivyo vingi viko mijini;

c) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuchukulia hatua kali kwa makandarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango kwani yapo majengo na barabara nyingi zilizojengwa chini ya viwango kwani Serikali inatumia fedha nyingi za walipa kodi kuweza kugharamia miradi hii; Mfano, barabara ya Dodoma –Iringa imeanza kuharika huku haina muda mrefu tangu ijengwa.

d) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa Ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha Makandarasi wazalendo kujiunga na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia Mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wadogo na wa kati;

e) Wakati Serikali inajenga barabara pamoja na mambo mengine kuzingatia vigezo muhimu kiuchumi, kijamii (hasa huduma za afya na elimu) pamoja na ahadi za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani;

f) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama Runinga, Magazeti, Redio na Simu za Mkononi. Pia vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

g) Serikali kuharakisha kuleta Sheria bungeni ya Vyuma Chakavu ili kuweza kusaidia kupambana na watu wachache waliokosa uzalendo ambao wanaiba vyuma zenye alama za barabarani na kuviuza kama vyuma chakavu. Vilevile, kuchukuwa hatua kali za kulipa faini kwa magari ambayo yanagonga vibao vya alama barabarani;

h) Serikali iendelee na juhudi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;

i) Serikali kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (*One Stop Inspection Stations*) ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;

j) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara kuhakikisha wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo kwani maeneo mengi ambayo mifugo inatumia kuvuka kumekuwa na uhalibifu mkubwa sana wa barabara;

k) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa makandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vya maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira) pamoja na ushuru unaotozwa na Halmashauri za miji;

   Gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa barabara hivyo Kamati inaishauri Serikali kusamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi; na

l) Serikali kuendelea kutoa kazi za ujenzi wa barabara kwa wakandarasi wazawa ilikuweza kuongeza ujuzi na uzoefu katika shughuli za ujenzi.

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na hasa jengo la abiria ni jambo la kimkakati katika kuchochea uchumi wa nchi hivyo; Kamati inashauri Serikali kuweka kipaumbele na kuchukuwa hatua za makusudi kutekeleza azma yake ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ikiwa ni pamoja na kuharakisha ujenzi wa jengo la abiria ili kuweza kuendana na viwango vya Kimataifa ambavyo vimeainishwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga- ICAO kuwa sharti moja wapo ni kuwa abiria wa ndani na wa nje hawaruhusiwi kuchanganyika katika eneo moja;

b) Serikali kukamilisha kwa haraka ujenzi wa Jengo la Tatu (*Terminal III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa. Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi;

c) Serikali kutoa fedha zote zilizoidhiniwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;

d) Serikali kuhakikisha inapata Hati Miliki za mali zake zote hususan viwanja vya ndege. Hii iambatane na kuweka mipaka, uzio au nguzo kuepusha uvamizi na migogoro kwa wananchi wanaoishi kandokando ya viwanja vya ndege; na

e) Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Viwanja vya ndege hasa mifereji ili kuzuia maji/ mafuriko kutuhama katika viwanja vya ndege hasa wakati wa mvua na kusababisha ndege kushindwa kuruka ama kutua.

3) **Mhesimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Majengo –TBA, Kamati inashauri yafuatayo:-
   a) Serikali kuimarisha uwezo wa Wakala wa Majengo Tanzania-TBA ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia Pato la Serikali. Ni vyema Wakala huu pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu, kuhakikisha zinakuwa katika hali ya ubora na viwango vinavyostaili;

   b) Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa majengo ya Serikali, ni vema sasa Wakala wa Majengo Tanzania kuanza kushirikiana na taasisi zingine za Serikali zinazohusika na ujenzi kama Suma JKT, Shirika la Nyumba la Taifa na zingine ili kuongeza kasi ya ujenzi na kuleta tija;

   c) Wakala wa Majengo nchini kufanya ukarabati wa nyumba zake zilizo maeneo mbalimbali ya nchi kwani nyingi ziko katika hali isiyoridhisha hasa kwenye mifumo ya umeme na maji machafu na hivyo kuhatarisha maisha ya wapangaji;

   d) Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye majengo ya Ikulu ndogo zilizopo kwenye Wilaya mbalimbali nchini kote; na

   e) Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha ili kuongeza usimamizi wa miradi mingi na mikubwa inayosimamiwa na Wakala huu;

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme- TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Wakala wa Ufundi na Umeme kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna Wilaya zingine ziko umbali mrefu kwenda Makao Makuu ya Mkoa;

b) Wakala kuchukuwa hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo kwa kiasi kikubwa inazidai taasisi za Serikal ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na

c) Serikali kuajiri wataalaum waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

### 3.3 Sekta ya Mawasiliano

1) **Mheshimiwa Spika,** ufuatao ni ushauri wa Kamati kuhusu Sekta ya Mawasiliano;

   a) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wake kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania kwa kufunga ''moduli'' ya uhakiki mapato ya huduma za mawasiliano ijulikanayo kama (*Telecom Revenue Assurance System* (*TRAS*). Hii itasaidia Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya kodi stahiki kutoka kwa makampuni ya simu kwa miamala inayofanyika;

   b) Serikali kutoa fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwani sekta hii inachangia kiasi kikubwa cha fedha kwenye mfuko mkuu ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha **shilingi bilioni 10.9** zilikusanywa kutoka kwenye mkongo na **shilingi bilioni 8.7** zilikusanywa kutoka Mamlaka ya mawasiliano;

   c) Kwa kuwa Serikali inamiliki asilimia 40 ya hisa za Kampuni ya Airtel Tanzania; na kwa kuwa tangu ilipoingia ubia Serikali haijawahi kupata gawio; Kamati inasisitiza suala hili kuangaliwa kwa umakini;

d) Serikali kuipa kipaumbele mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

e) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao;

f) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kama vile, uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya uhalifu wa kimtandao na kuwabana wahalifu; na

g) Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao.

4.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, sekta hii ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

4.1 **Shukrani**

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, (Mb) akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Eng. Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb).

Vile vile, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuhanga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Angelina Madete. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalam wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb - ‵′

5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb - ‵′
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb - ‵′
7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb - ‵′
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb- ‵′
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb - ‵′
10. Mhe. Nuru Awadh Bafadhil, Mb - ‵′
11. Mhe. James Francis Mbatia, Mb - ‵′
12. Mhe. Saul Henry Amon, Mb - ‵′
13. Mhe. Ahmed Makhbuty Shabiby - ‵′
14. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb - ‵′
15. Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb- ‵′
16. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfed Kikwembe, Mb-‵′
17. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb - ‵′
18. Mhe. Dua William Nkurua, Mb - ‵′
19. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb - ‵′
20. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb - ‵′
21. Mhe. Charles Kitwanga, Mb - ‵′
22. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb - ‵′
23. Mhe. Rukia Kassim, Mb - ‵′
24. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - ‵′

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson M. Bisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Hosiana John na Ndg. Richard Masuke pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya M

apato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, (Mb)
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**

23 Aprili, 2017